BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA SHERIA, UTAWALA BORA NA IDARA MAALUM KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo, kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena, asubuhi ya leo, katika Mkutano huu wa sita kwa dhamira ya kujadili Bajeti kuu ya Seriakali na Taasisi zake, chini ya Baraza lako Tukufu. Kwani hii ni rehma yake Muumba kwa kutupa pumzi na afya njema ambayo wenzetu wengine amewanyima.

**Mheshimiwa Spika;** Aidha, kwaniaba ya Kamati yangu, naomba kutoa pole kwa wale wote walioathirika na mvua za masika ambazo zinaendelea kunyesha katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Tunaomba wananchi waendelee kuchukua tahadhari na maradhi ya miripuko kwa kuimarisha mazingira yetu kwa kuweka safi ili yawe salama kwa mda wote ambao mvua zinaendelea kunyesha pamoja na kuelimisha jamii yetu juu ya athari zinazoweza kutokea na kupelekea maafa.

**Mheshimiwa Spika;** Vile vile niendelee kutoa pole kwa wakaazi wa Pangawe, Kinuni na Nyarugusu kwa upepo mkali uliotokea jana majira ya asubuhi na kuathiri nyumba za wananchi wa maeneo hayo na miundombinu ya maendeleo. Kamati inawaomba waathirika wote wa maafa hayo kuwa na moyo wa ustahamilivu na sisi viongozi wao tuko pamoja nao kwa kipindi hiki kigumu.

**Mheshimiwa Spika**, Vile vile, nadhani sitokuwa mwingi wa fadhila bila ya kushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya **Sheria,**

**Utawala Bora na Idara Maalum** kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Pia napenda niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati Waziri Mhe. Haji Omar Kheir, Naibu Waziri, Mhe. Shamata Shaame Khamis, Nd. Katibu Mkuu pamoja Afisa Mdhamini Pemba, na watendaji wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha katika Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wakuu, Maafisa na Wapiganaji wote wa Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yao waliyotupatia kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Sambamba na hayo, napenda kutoa shukrani kwa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kuwasilisha mbele ya Kamati, pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha, kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 ili ipate Baraka za Wajumbe wako na kwa mnasaba huo, tunaomba ipitishwe kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika;** Aidha, nitoe shukrani na pongezi za pekee kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi imara wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kusimama vyema katika uongozi wake na kuhakikisha maslahi ya Watumishi wa Umma yameboreshwa.

**Mheshimiwa Spika;** Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa maboresho haya ni Utekelezaji nzuri wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ambapo utekelezaji wake utaendelea kwa kipindi chote cha Bajeti ya mwaka 2017/2018 na kuhakikisha kuwa hatua kubwa ya maendeleo inafikiwa ili kuwezesha jamii kiuchumi na kujikwamua na umasikini.

**Mheshimiwa Spika**, pia naomba kuwashukuru kwa kazi kubwa walioifanya Wajumbe wa Kamati yetu wakati tukiwa tunapitia bajeti hii, kwa kuonesha mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu haya ambayo yanaiwezesha kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Hivyo, kwa ridhaa yako naomba uwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said — Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa — Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir — Mjumbe
5. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf — Mjumbe
6. Mhe. Ali Khamis Bakar — Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Makame Ali — Mjumbe

Pamoja na Makatibu wetu waliosaidia sana kufanikisha kazi hii, ambao ni **Ndg. Rahma Kombo Mgeni** na **Ndg. Ali Alawy Ali.**

**Mheshimiwa Spika:**

Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Iadara Maalum imeweza kuchambua na kujiridhisha vyema katika kupitia Fungu la Bajeti ya wizara hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 96(1) na 106(3) katika jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2016.

**Mheshimiwa Spika;** Kupitia Bajeti hii ya mwaka 2017/2018 wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imeazimia kutekeleza vipaumbele vinne ambavyo vinalengo la:-

(i) kuimarisha ulinzi na usalama kwa wenyeji na wageni kwa kufunga vifaa vya ulinzi katika maeneo ya mji, kuanzisha wakala wa ulinzi na kununua boti za doria;
(ii) kutekeleza mkakati wa upelekaji madaraka kwa wananchi (Ugatuzi) kwa kufanya shughuli mbali mbali ikiwemo suala la kutoa elimu ya ugatuzi kwa wananchi, viongozi na taasisi mbali mbali;
(iii) kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika Idara na Taasisi za ofisi, pamoja na;
(iv) Kuimarisha makaazi na majengo ya Ofisi za Idara Maalum.

**Mheshimiwa Spika;** Ni imani yangu kwamba kupatiwa fedha zilizotengwa kwa wizara hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji na ukamilishaji wa vipaumbele vya malengo hayo waliokusudia kwa mwaka ujao, ambapo Kamati inatia mkazo zaidi katika uimarishaji wa makaazi na majengo ya ofisi za Idara Maalum, kwa kuwa tumeona katika vituo mbali

mbali jinsi tatizo hili lilivyoshamiri na kuweza kurudisha nyuma maendeleo yao.

**IDARA ZA MAKAO MAKUU**

**Mheshimiwa Spika;** katika kutekeleza kazi zake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati yangu imefanikiwa kutembelea na kujionea shughuli mbali mbali za kawaida na zile za miradi ya maendeleo ambazo zinasimamiwa na kuratibiwa na wizara hii katika utekelezaji wake, ikiwa zimekabiliwa na changamoto kadhaa kama vile udogo na ukomo wa Bajeti ambayo haikidhi mahitaji ya Idara husika.

**Mheshimiwa Spika;** kamati yangu inashauri kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Idara hizi kupatiwa fedha za kutosha na kwa wakati ili kuweza kutatua changamoto ambazo zinawakwaza katika uendeshaji wa shughuli zao, kwa lengo la kuleta ufanisi na kuimarisha sekta zote za maendeleo.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

**Mheshimiwa Spika,** Mbali ya majukumu iliyopangiwa idara hii ikiwemo kusimamia sera, mipango na programu za wizara lakini pia, ina jukumu la ufatiliaji wa tathmini za programu na miradi. Ni imani ya kamati yangu kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Idara hii itaweza kupatiwa fedha za kutosha ili kufanya shughuli zake kama inavyotakiwa.

**OFISI YA AFISA MDHAMINI - PEMBA**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba, ofisi imefanikiwa kuendelea kuratibu na kusimamia majukumu yake kama ilivyo. Hivyo, Kamati yangu inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuwaingizia fedha vizuri kwa mwaka huu, kitu ambacho kimeleta faraja katika utekelezaji wa majukumu yake, kwa kuwa wao ni kiungo muhimu katika utekelezaji na usimamizi wa kazi za wizara hii kwa upande wa Pemba.

**IDARA MAALUM ZA SMZ**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara maalum za SMZ, Kamati inapongeza sana juhudi zinazofanywa na wapiganaji wetu wa vikosi hivi kwa kazi ngumu wanayoifanya ya kulinda usalama na kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu katika Nchi yetu.

Samba samba na hayo, Kamati katika ziara zake tofauti iliweza kubaini changamoto mbali mbali zinazorudisha nyuma maendeleo ya Idara hizi kama vile:- Kuwepo kwa majengo na vitendea kazi ambavyo havikidhi haja ya askari wetu; Kuwepo kwa upungufu wa sare (uniform) za askari; na Kuwepo kwa ukosefu wa Hatimiliki zaidi kwa upande wa vituo vya Pemba. Aidha, changamoto kubwa katika vikosi kama vile JKU, KZU na Mafunzo ni kuishiwa na Bajeti za matumizi mapema na kusababisha vikosi hivyo kushindwa kutekeleza malengo yao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati yangu inashauri katika Bajeti hii kuangaliwa zaidi kwa vikosi vyetu ambavyo vinatumika kila siku katika uimarishaji wa amani na usalama wa nchi na raia kwa ujumla. Aidha, Kamati inaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanya mabadiliko ya maslahi kwa vikosi vyetu, hivyo mabadiliko hayo yatajenga hamasa na kuamsha ari ya kujituma zaidi katika kupigania maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika;** kamati yangu inapongeza sana juhudi za Wizara kwa uanzisha Uwakala wa Idara Maalum kama ambavyo wenzetu wa JKT wanavyo tumia uwakala wa SUMA JKT katika kuratibu shughuli zao mbali mbali za uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaomba kupitia Bajeti hii waidhinishiwe fedha zote walizoomba na pia, jitihada zifanyike kwa kuhakikisha kwamba wanapatiwa fedha za kutosha ambazo zitawaendesha mpaka mwisho wa mwaka wa fedha na kuingiziwa kwa wakati, ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

## JESHI LA KUJENGA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika;** Jeshi la kujenga Uchumi ni miongoni mwa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo jukumu lake kubwa ni kutoa mafunzo kwa vijana katika Nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Dhamira ya JKU ni kuchangia kuimarisha uchumi kwa kutoa mafunzo ya uzalishaji, ufundi na kazi za amali, mila, utamaduni na uzalendo. Hivyo, dhamira hii ya JKU itakamilishwa kupitia Programu Kuu mbili, ambazo ni Programu ya Mafunzo kwa vijana na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa JKU.

**Mheshimiwa Spika;** Aidha, Kamati yangu imebahatika kutembelea vituo mbali mbali vya JKU Unguja na Pemba na kujiridhisha na utendaji wao kwa lengo la kusaidia Serikali kunyanyua maendeleo ya nchi. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto kubwa ya uchakavu wa mahanga ya kulala askari na vijana ambao wanajitolea kujenga Taifa, changamoto ambazo zinaikabili Idara hili katika vituo vya Msaani, Chambani pamoja na Kangani kwa upande wa kisiwa cha Pemba.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitisha fungu liliombwa kwa ajili ya kuendesha shughuli mbali mbali za Jeshi hili, ili kuweza kukamilisha malengo yao waliyojipangia.

## CHUO CHA MAFUNZO ZANZIBAR

Chuo cha Mafunzo ni Idara ambayo ina jukumu kubwa la kuwapokea wale wote wanaopelekwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa Sheria, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha tabia ili wanaporejea katika jamii wawe raia wema. Urekebishaji unajumuisha fani mbali mbali za kazi za mikono, ujenzi, ushoni, ufundi magari, ufundi kuchonga pamoja na huduma za ushauri nasaha. Ili kuweza kufanikisha majukumu hayo, Chuo cha Mafunzo kimepanga programu kuu mbili, ambazo ni Huduma za urekebishaji Wanafunzi wa Chuo cha Mafumzo na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Chuo cha Mafunzo.

**Mheshimiwa Spika;** Katika ziara iliyofanywa na Kamati katika vituo vyake, imeona kushamiri kwa changamoto kadhaa ambazo ni vyema kwa

Bajeti hii zikaweza kupatiwa ufumbuzi. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa uchakavu wa majengo ya ofisi, ubovu wa nyumba za kuishi askari pamoja na uchakavu wa jela za wanafunzi, kuwepo kwa tatizo la ukosefu wa Hatimiliki za maeneo ya Kambi pamoja na mashamba wanayotumia kwa ajili ya kilimo, ukosefu wa usafiri wa uhakika takribani katika vituo vyote vya Unguja na Pemba; kuwepo kwa tatizo la huduma za afya ikiwemo ukosefu wa madawa na wahudumu wa afya.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati yangu inashauri katika mwenendo mzima wa upatikani wa fedha za matumizi kwa mwaka unaokuja, Chuo cha Mafunzo kipewe kipaumbele kwa kuimarisha makaazi, ofisi zao na huduma za afya, katika matumizi ya fedha ambazo zitaidhinishwa katika mwaka huu wa 2017/2018. Aidha, Kamati inashauri endapo hali ya kifedha itaruhusu, kuongezwa fungu la Chuo cha Mafunzo ili kutafutia vitendea kazi ambavyo vitasaidia katika uendeshaji wa kiwanda chao cha ushoni na uchongaji kilichopo katika kambi ya Kilimani.

## KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

**Mheshimiwa Spika;** Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kina jukumu la kuhakikisha kuwa kinazuia usafirishaji wa mali yoyote ambayo imezuiwa kisheria kusafirishwa baharini na nchi kavu kwa namna yoyote kutoka nje ya mipaka ya Zanzibar. Aidha, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kikosi hiki kwa mwaka wa fedha ujao kimepanga kutekeleza Programu kuu mbili; ambazo ni Programu ya Ulinzi na Usalama na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imeona kuwepo kwa tatizo la upungufu wa mahanga ya kulala askari wake pamoja na Kamandi ya Pemba kukosa Hatimiliki za maeneo ya vituo vyake mbali mbali kiasi kwamba baadhi ya maeneo huingiliana kwa shughuli za kambi na wananchi, mfano mzuri ni kambi ya Makombeni. Aidha, Kamati inashauri kwa Kambi hii Serikali itoe fidia kwa wamiliki wa shamba lililopo ndani ya kambi ambao wanasababisha muingiliano na shughuli za kambi, ili kuwa huru kwa kambi hii ambayo umiliki wa eneo lake unaleta wasiwasi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati yangu inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza Bajeti ya kikosi hiki ili kuweza kununua na kurudisha tena matumizi ya Rada kwa kikosi cha Sengenya kisiwani Pemba, kwa lengo kuimarisha hali ya ulinzi na usalama wa Baharini na Nchi kavu.

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI**

**Mheshimiwa Spika;** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kina lengo la kutoa huduma za kuzima moto na uokozi kwa ufanisi pamoja na kutoa elimu ya Zimamoto na uokozi kwa wananchi, Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi juu ya kinga na hadhari za moto. Aidha, KZU kimepanga Programu kuu mbili ambazo zitawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao, ambayo ni Programu kuu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi; na Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Zimamoto na Uokozi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati yangu inasikitishwa sana na hali ya makaazi kwa baadhi ya vituo kwa Unguja na Pemba, kwa kuona hakuna kabisa mahanga ya kuishi askari na hivyo hulazimika kujibana katika sehemu zao za ofisi jambo ambalo ni hatari kwa afya ya binadamu. Hali hii ilionekana katika vituo vya Mwanakwerekwe, Mahonda, Wete, Uwanja wa Ndege Kisiwani Pemba na Malindi – Bandarini. Kwahivyo, Kamati inaomba wizara kwa kushirikiana na wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutenga eneo maalum ambalo litakuwa na usalama kwao kwa ajili ya Kikosi cha Zimamoto pale Bandarini, ili kuepuka usumbufu na msongamano wa magari katika eneo lile wakati linapotokea tatizo.

**Mheshimiwa Spika;** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, pia kinakabiliwa na tatizo la kumalizika kwa Bajeti yake mapema kutokana na ufinyu na ukomo wa Bajeti yake, hivyo kupelekea kuzorota kwa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Vile vile, inashuri wizara husika kwa mashirikiano na Mamlaka ya viwanja vya ndege kuweka miundombinu bora ya mawasiliano kwa kujenga na barabra ndani ya maeneo ya uwanja wa ndege ili kuwezesha kazi za zimamoto kufanyika kiufanisi.

**Mheshimiwa Spika;** kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya ununuzi wa vifaa vya zimamoto kama vile nguo maalum za kuzimia moto. Pia, Kamati inatia mkazo lengo la Serikali la kujenga kituo cha Zimamoto kila

Wilaya, Hivyo tunaomba azma hii ya Serikali itekelezwe na kwa wakati kama ilivyopangwa.

Aidha, Kamati inashauri kuongezwa kwa fungu la matumizi au Serikali kuchukua hatua mbadala za kupatiwa fedha kwa kikosi hiki, ambacho kimepangiwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, licha ya kuwa ni tofauti na fungu la mwaka jana ambalo lilimalizika kabla ya robo ya tatu ya utekelezaji wa Bajeti yake.

## KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)

**Mheshimiwa Spika;** Jukumu la KVZ ni kuweka amani na utulivu katika nchi; kupambana na janga lolote litakaloikumba jamii; kulinda viongozi na mali za Serikali na kufanya kazi za kijeshi kwa lengo la kulinda hali inayohatarisha usalama wa Taifa. Aidha, Kikosi kimejipangia kutekeleza programu kuu mbili katika Bajeti hii ya 2017/2018 ambazo ni Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao, na Programu ya Uendeshaji na Utawala wa Kikosi Cha Valantia.

**Mheshimiwa Spika;** Katika ziara iliyofanywa na Kamati kupitia vituo vyote vya Unguja na Pemba, iliweza kujionea maendeleo ya shughuli zao ambazo zimekumbwa na changamoto mbali mbali kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika;** katika utekelezaji wa kazi zake, Kamati imebaini ukosefu wa majengo ya ofisi na mahanga ya askari imekuwa tatizo kubwa la Kikosi hiki kwa kambi zake mbali mbali za Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inashauri kupatiwa bajeti yao kama walivyoomba na kuingiziwa kwa wakati, ili kuweza kusaidia kutatua tatizo hili pamoja na kufanya ukarabati wa majengo hususan kambi ya Ndugukitu iliyopo Chake-Chake Kisiwani Pemba. Pia, Kamati inaomba kwa taasisi zote za Serikali zenye madeni katika Kikosi hiki, basi walipe kama mikataba yao inavyoelekeza katika kazi husika.

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## MKOA WA MJINI MAGHARIBI

**Mheshimiwa Spika**, Mkoa wa Mjini Magharibi umeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo la utekelezaji wa sera, sheria, mipango na miongozo ya Serikali ndani ya Mkoa huo. Aidha, Mkoa wa Mjini Magharibi umedhamiria kutekeleza programu kuu tatu katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, kwanza, ni programu kuu ya kuimarisha shughuli za Serikali katika Mkoa, Uendeshaji na Uratibu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, na tatu ni Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwa uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi kujipanga vizuri katika kukabiliana na maradhi ya miripuko kama kipindupindu na mafuriko ya mara kwa mara hali ambayo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na ujenzi holela katika mkoa huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Baraza la Manispaa kamati yangu inatoa pongezi kwa Baraza la Manispaa kwa kusafisha mji zaidi katika kipindi hichi cha mvua za masika zinazoendelea kunyesha katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Vile vile, kamati inashauri Halmashauri kuajiri watumishi wa kudumu badala ya kuajiri kwa mkataba wa mda mfupi hasa katika sekta za fedha. Hata hivyo, Kamati inashauri wakati wa kuajiriwa watumishi wa kudumu au kuhamishiwa watumishi basi Manispaa isiwe ndio sehemu ya kupelekwa watumishi waliokosa sifa nzuri huko wanakotoka, yaani kufanywa Manispaa ni *Sehemu ya kuwekea takataka.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inazishauri Halmashauri zote za Unguja na Pemba, kuweka utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki badala kukusanya mapato kwa utaratibu uliozoeleka. Vile vile, Kamati inashauri wananchi wawe na tabia ya kudai na kutoa risiti wakati wa kufanya manunuzi ili kulinda mapato ya Serikali. Njia hii itasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa mapato yanayokusanywa kupitia vyanzo mbali mbali.

**MKOA WA KUSINI – UNGUJA**

Mkoa wa Kusini – Unguja umefanikiwa kufuatilia shughuli zake mbali mbali za kimaendeleo ikiwemo huduma za kiafya, elimu, maji, kilimo na shughuli mtambuka kwa vijana. Aidha, Kamati inampongeza Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja kwa juhudi zao wanazochukuwa kukabiliana na uingizwaji wa madawa ya kulevya katika maeneo yake kupitia baharini na nchi kavu. Pia, Kamati yangu imeridhishwa na utaratibu wake wa kuboresha maendeleo ya elimu ya msingi katika wilaya hii.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mkoa huu umejipanga kutekelza programu kuu tatu ambazo zitasaidia kuimarisha hali ya maendeleo kwa wakaazi wa Mkoa huu.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inashauri uongozi wa Mkoa wa Kusini wasichoke katika kukabiliana na kesi za udhalilishaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia wizara ya fedha kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri za Mkoa huu, kwani zipo sehemu ambazo mpaka mda huu mapato yanayokusanywa hayaridhishi kwa namna yanavyokadiriwa.

**MKOA WA KASKAZINI – UNGUJA**

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imeelezwa kuwa ofisi ya Mkoa imeendelea na kufanya shughuli zake za kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta mbali mbali za kijamii kama vile maji, elimu, afya, kilimo na mazingira, watu wenye ulemavu, wanawake na watoto na ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika;** Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hiki, Kamati imeelezwa kushamiri kwa kesi za udhalilishaji na ukatili zikiwaathiri zaidi wanawake na watoto. Aidha, Kamati inashauri kupitia Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa Mkoa, Wilaya na Shehia kuandaliwe mpango maalum wa kukomesha kesi hizi za udhalilishaji kwa watuhumiwa kufikishwa katika vyombo vya Sheria.

## MKOA WA KASKAZINI – PEMBA

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inashauri kwa Mkoa huu taasisi ambazo zinawajibu wa kukusanya mapato kuhakikisha lengo na dhamira ya uwepo wake limekamilika, pia ufuatiliaji na usiamamiaji mzuri wa ukusanyaji mapato umeboreshwa. Aidha, kwa mwaka uliopita ukusanyaji wa mapato haukuwa wa kuridhisha.

Hivyo, Kamati inashauri kwa mwaka mpya unaokuja kutilia mkazo zaidi ukusanyaji wa mapato bila kuoneana muhali na zaidi kwa vile wamengezewa chanzo cha mapato cha soko kuu la mji wa Wete.

## MKOA WA KUSINI – PEMBA

**Mheshimiwa Spika;** Kamati iliweza kufanya ziara zake tofauti katika Mkoa wa Kusini Pemba na kuona ni miongoni mwa taasisi muhimu zinazosaidia kuchangia mapato ya Serikali kupitia Mabaraza yake ya mji wa Ckake-Chake na Mkoani. Mkoa huu umejitahidi sana kuboresha huduma za kijamii kama vile maji, afya, elimu, umeme na barabara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017. Pia, Mkoa umeendelea kuratibu na kusimamia majukumu ya sekta mbali mbali ambazo zimo ndani ya Mkoa huu.

**Mheheshimiwa Spika;** Kamati inashauri uongozi wa Mkoa wa Kusini Pemba kuajiri wafanyakazi wa mkataba yaani wataalamu mbali mbali ambao wataweza kusaidia katika ukusanyaji wa mapato.

## AFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mabadiliko mapya yaliyofanywa na Serikali kwa kuwekwa pamoja afisi ya usajili wa vizazi, vifo na kadi za utambulisho, kwa ajili ya kuleta ufanisi katika majukumu yao kwa vile yanalingana kiutendaji pamoja na kukamilisha lengo la Serikali la kuwa na rikodi ya taarifa za mtu tokea anazaliwa hadi anafariki.

**Mheshimiwa Spika,** kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kwa kuendelea kusajili vizazi na kutoa vyeti kwa kutumia mfumo wa

elektroniki, hali ambayo kamati imeona ni vyema kuendelea kutumika kwa Wilaya nyengine za Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika;** kwa kuwa hali ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/2017 haukuwa wa kuridhhisha na ni asilimia 25 tu mpaka kufikia mwezi wa March 2017, basi Kamati inashauri katika fungu kuu la Seriakali kuangalia Ofisi hii ya Mrajisi wa vizazi na vifo na Kadi za Utambulisho ili kuweza kufikia malengo waliokusudia.

Vile vile, Kamati inapendekeza kwa Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kupatiwa fungu fulani la fedha ambazo wanakusanya kupitia ofisi yake ili kusaidia katika uendeshaji wa shughuli zao.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum mbele ya Baraza lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika;** kwa niaba ya Kamati yangu naomba Waheshimiwa Wajumbe waichangie, waijadili na waiboreshe hotuba hii na mwishowe waidhinishie bajeti hii, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, makadirio ya Matumizi ya jumla ya Shilingi 122,322,494, 273/= zikiwemo Shilingi 82,897,900,000/= kwa kazi za kawaida na Shilingi 28,320,000,000/= kwa kazi za Maendeleo katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Aidha, Kamati yangu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuridhia Mchnago wa Ofisi hii wa jumla ya Shilingi 629,090,000/= ikiwa ni mapato yatakayoingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** **Kwa niaba ya Kamati yangu Naunga Mkono Hoja.**

**Ahsante;**

...............................

(Mwantatu Mbaraka Khamis)

Kny: Mwenyekiti,

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**